



MUHTASARI WA PATO LA TAIFA
ROBO YA KWANZA (JANUARI - MACHI) 2023
BEI ZA MWAKA WA KIZIO 2015



Ofisi ya Taifa ya Takwimu
Wizara ya Fedha
Juni 2023

Yaliyomo

Majedwali	iii
Orodha ya Vielelezo	iv
Viambatisho	v
1.0 Utangulizi.....	2
1.1 Uchumi wa Dunia	2
1.2 Nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara	2
1.3 Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika	2
1.4 Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki	3
1.5 Ukuaji wa Uchumi Nchini Tanzania	4
1.5.1 Pato la Taifa, Robo ya Kwanza Mwaka 2023	4
1.5.2 Mchango katika Pato la Taifa Robo ya Kwanza, Mwaka 2023	5
1.5.3 Ukuaji wa Shughuli za Uchumi kipindi cha Robo ya Kwanza, Mwaka 2023	6
1.5.4 Mchango katika Kiwango cha Ukuaji Robo ya Kwanza, Mwaka 2023	7
2.0 Viwango vya Ukuaji kwa Shughuli za Kiuchumi	7
2.1 Kilimo, Misitu na Uvuvi	7
2.1.1 Mazao	7
2.1.2 Mifugo	8
2.1.3 Misitu.....	8
2.1.4 Uvuvi	8
2.2 Uchimbaji Madini na Mawe	8
2.3 Uzalishaji Viwandani	9
2.4 Umeme	9
2.5 Usambazaji Maji	10
2.6 Ujenzi	11
2.7 Biashara na Matengenezo	11
2.8 Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo	11
2.9 Malazi na Huduma za Chakula.....	12
2.10 Habari na Mawasiliano	12
2.11 Fedha na Bima	12
2.12 Upangishaji Majengo	13
2.13 Shughuli za Kitaalam, Ufundi na Sayansi	13
2.14 Huduma Zinazohusiana na Utawala.....	14
2.15 Utawala na Ulinzi	14
2.16 Elimu	14
2.17 Afya.....	15
2.18 Huduma Nyingine za Jamii	15
3.0 Hitimisho	15

Majedwali

Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Madini Robo ya Kwanza, Mwaka 2019 – 2023	9
---	---

Orodha ya Vielelezo

Kielelezo Na 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Robo ya Kwanza Mwaka 2018 - 2023	4
Kielelezo Na. 2: Kiwango cha Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Kwanza Mwaka 2019 – 2023.....	5
Kielelezo Na. 3: Mchango katika Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Husika	6
Kielelezo Na. 4: Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo ya Kwanza, Mwaka 2023	6
Kielelezo Na. 5: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao Robo ya Kwanza, Mwaka 2022 na 2023.....	7
Kielelezo Na. 6: Uzalishaji Maji (Mita za Ujazi Milioni) Robo ya Kwanza, Mwaka 2019 – 2023.....	10
Kielelezo Na. 7: Thamani ya Mikopo na Amana (Sh. Trilioni), Robo ya Kwanza, Mwaka 2019 – 2023.....	13

Viambatisho

Kiambatisho Na. 1: Pato la Taifa kwa Shughuli za kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni	16
Kiambatisho Na. 2: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za mwaka 2015 – Asilimia	18
Kiambatisho Na. 3: Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Soko (Bei za Miaka inayohusika) – Sh. Milioni	20
Kiambatisho Na. 4: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa kwa Bei za Soko (Bei za miaka inayohusika) – Asilimia	22

1.0 Utangulizi

Pato la Taifa kwa robo mwaka ni kiashiria chenye taarifa za kina za mwenendo wa shughuli za uchumi. Kiashiria hiki hutumika katika kutathmini mwenendo wa shughuli za uchumi kwa vipindi vifupi vifupi kwa lengo la kutunga na kutathmini sera za kiuchumi kwa wakati muafaka katika nchi.

1.1 Uchumi wa Dunia

Kwa mujibu wa ripoti ya hali ya uchumi wa dunia iliyotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF) ya mwezi Aprili 2023, uchumi wa dunia ulikadiriwa kukua kwa kiwango cha asilimia 2.8 ikiwa ni pungufu kwa kiwango cha pointi za asilimia 0.1 ikilinganishwa na kiwango kilichokadiriwa kwenye Maoteo yaliyofanyika mwezi Januari 2023 ambayo yalikadiria ukuaji wa asilimia 2.9.

Kupungua kwa kasi ya ukuaji kumetokana na sababu mbalimbali ikiwemo: kuendelea na utekelezaji wa sera za kubana matumizi miongoni mwa nchi zilizoendelea pamoja na udhibiti wa mikopo inayoweza kusababisha kushindwa kukabiliana na changamoto mpya zinazojitokeza kwenye chumi mbalimbali duniani ambayo itachangia kupungua kwa pato ghafi la dunia kwa kiwango cha pointi za asilimia 0.3 mwaka 2023. Kiwango cha deni la Dunia kimeendelea kuwa cha juu hivyo kupunguza uwezo wa watunga sera kubuni mbinu za kukabiliana na changamoto mpya zinazojitokeza.

1.2 Nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara

Ukuaji wa uchumi wa nchi zilizo kusini mwa Jangwa la Sahara ulikadiriwa kuongezeka kwa kiwango cha asilimia 3.6 mwaka 2023 ambacho ni sawa na kupungua kwa asilimia za pointi 0.2 ukilinganishwa na makadirio yalifanyika kwenye Maoteo ya mwezi Januari 2023 yaliyokadiriwa kiwango cha ukuaji wa asilimia 3.8. Uchumi wa nchi ya Afrika Kusini ulikadiriwa kukua kwa kiwango cha asilimia 0.1 mwaka 2023 sawa na upungufu wa asilimia za pointi 1.1 kutoka kadirio la 1.2 asilimia lililokuwa limekadiriwa kwenye ripoti ya Januari 2023. Uchumi wa Nigeria umekadiriwa kuongezeka kwa asilimia 3.2 kama ulivyokadiriwa kwenye Maoteo yaliyofanyika mwezi Januari 2023.


1.3 Nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika

Kwa mujibu wa ripoti ya makadirio ya ukuaji wa uchumi mwezi Aprili 2023 inayotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF), ukuaji wa uchumi katika nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika unatarajiwa kukua kwa asilimia 3.6 mwaka 2023 ikiwa ni pungufu kwa pointi za asilimia 0.2 ikilinganishwa na maoteo yaliyofanyika mwezi Januari 2023.

Ukuaji wa uchumi kwa baadhi ya nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika. Uchumi wa nchi ya Afrika kusini umeongezeka kwa kiwango cha asilimia 0.4 kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 1.9 kipindi kama hicho mwaka 2022. Uchumi wa Namibia uliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.0 katika robo ya kwanza

mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 7.3 kipindi kama hicho mwaka 2022. Uchumi wa Botswana ulikua kwa kiwango cha asilimia 5.4 katika robo ya kwanza mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 6.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, uchumi wa Tanzania umeongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.6 katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.5 kipindi kama hicho mwaka 2022.

Kielelezo Na. 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za SADC, Robo ya Kwanza 2022 na 2023




Chanzo: Tovuti za Ofisi za Takwimu za Nchi Husika, 2023

1.4 Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki ambazo zimetoa taarifa za mwenendo wa shughuli za uchumi katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023 zilizopatikana kwenye wavuti za taasisi hizo zimeonesha kuendelea kuimarika kwa ukuaji chanya wa uchumi ambapo kiwango cha ukuaji kwa nchi ya Rwanda umeongezeka hadi asilimia 9.2 ikilinganishwa na asilimia 7.9 kipindi kama hicho mwaka 2022. Uchumi wa Uganda umekua kwa kiwango cha asilimia 4.9 katika robo ya kwanza mwaka 2023 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 5.1 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, uchumi wa Tanzania umekua kwa kiwango cha asilimia 5.6 ukilinganishwa na asilimia 5.5 katika robo ya kwanza mwaka 2022. Nchi nyingine Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki bado hazijatoa taarifa za mwenendo wa ukuaji wa uchumi katika kipindi cha mwezi Januari hadi Machi 2023.

Kielelezo Na 1: Ukuaji wa Uchumi kwa Baadhi ya Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki, Robo ya Kwanza Mwaka 2018 - 2023



Chanzo: Tovuti za Ofisi za Takwimu za Nchi Husika, 2023

1.5 Ukuaji wa Uchumi Nchini Tanzania

Utayarishaji wa Takwimu za Pato la Taifa katika kipindi cha robo ya kwanza (Januari - Machi) 2023 umetumia taarifa zilizokusanywa kutoka katika shughuli zote za kiuchumi zilizofanyika Nchini. Aidha, utayarishaji umezingatia Mwongozo wa Kimataifa wa Kutayarisha Takwimu za Pato la Taifa unaojulikana kama *2008 System of National Accounts*. Taarifa hii inahusu Pato la Taifa kwa Tanzania Bara kwa bei za mwaka husika na Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2015.

Ofisi ya Taifa ya Takwimu inaendelea kutekeleza Sera ya Mapitio ya Takwimu za Pato la Taifa iliyoanza kutumika mwaka 2019. Sera hii inaruhusu kuchapisha matokeo ambayo yanaweza kufanyiwa mapitio kutokana na kupatikana kwa takwimu mpya au zilizofanyiwa mapitio za kila robo mwaka na za kila mwaka. Kutokana na mapitio ya Sera hii na maboresho yaliyofanyika kwenye takwimu za urari wa biashara zinazotolewa na Benki Kuu ya Tanzania, takwimu za Pato la Taifa za mwaka 2017 - 2022 zimefanyiwa mapitio.


1.5.1 Pato la Taifa, Robo ya Kwanza Mwaka 2023

Katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023, Pato la Taifa kwa bei za mwaka husika (current prices) liliongezeka hadi Shilingi trilioni 46.5 kutoka Shilingi trilioni 41.5 kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, Pato la Taifa kwa bei za mwaka 2015 (constant prices) liliongezeka hadi Shilingi trilioni 36.9 katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023 kutoka

Shilingi trilion 34.9 katika kipindi kama hicho mwaka 2022, ikiwa ni sawa na ongezeko halisi la asilimia 5.6.

Kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa katika robo ya kwanza mwaka 2023 kunatoa fursa za kuhuisha sera za kodi zenye lengo la kuongeza mapato ya Serikali na pia kuongeza matumizi ya Serikali katika uwekezaji na sera ya fedha kwa ajili ya kuongeza ujazi wa fedha zinazohitajika katika uzalishaji bila kusababisha mfumuko wa bei na pia kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi ambayo ni injini ya ukuaji wa uchumi.

Kielelezo Na. 2: Kiwango cha Ukuaji wa Pato la Taifa, Robo ya Kwanza Mwaka 2019 – 2023




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2023

1.5.2 Mchango katika Pato la Taifa Robo ya Kwanza, Mwaka 2023

Mchanganuo wa mchango wa makundi makuu ya shughuli za kiuchumi katika Pato la Taifa katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023 unaonesha kuwa, Shughuli za Msingi zilikuwa na mchango mkubwa zaidi wa asilimia 39.7, zikifuatiwa na Shughuli za Huduma asilimia (38.9) na Shughuli za Kati asilimia (21.4). Mchango wa makundi makuu ya shughuli kuu za kiuchumi katika Pato la Taifa umekokotolewa kwa bei za mwaka husika kabla ya kujumuisha kodi.

Kielelezo Na. 3: Mchango katika Pato la Taifa kwa Bei za Miaka Husika




Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2023

1.5.3 Ukuaji wa Shughuli za Uchumi kipindi cha Robo ya Kwanza, Mwaka 2023

Katika kipindi cha Januari hadi Machi 2023, shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe iliongoza kwa ukuaji wa asilimia 14.2, ikifuatiwa na fedha na bima (asilimia 12.9), huduma ya chakula na malazi asilimia (12.3), huduma nyingine za jamii zinazojumuisha sanaa na burudani na shughuli za kaya katika kuajiri (asilimia 9.5), uzalishaji na usambazaji umeme (asilima 8.1), uzalishaji viwandani (asilimia 6.5), habari na mawasiliano (asilimia 6.4), ujenzi asilimia 6.2 na biashara na matengenezo (asilimia 6.0).

Kielelezo Na. 4: Viwango vya Ukuaji wa Shughuli za Uchumi, Robo ya Kwanza, Mwaka 2023



Chanzo: Ofisi ya Taifa ya Takwimu, 2023

1.5.4 Mchango katika Kiwango cha Ukuaji Robo ya Kwanza, Mwaka 2023

Shughuli zote za uchumi zilizofanyika katika kipindi cha Januari hadi Machi 2023 zilichangia katika ukuaji wa uchumi kwa kiwango cha asilimia 5.6 ikilinganishwa na asilimia 5.5 kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, shughuli za uchumi zilizokuwa na mchango mkubwa katika ukuaji huo zilikuwa ni pamoja na: kilimo (asilimia 15.9), ujenzi (asilimia 15.5), uchimbaji wa madini na mawe (asilimia 11.9), biashara na matengenezo (asilimia 9.1), uzalishaji viwandani (asilimia 9.0) na fedha na bima (asilimia 8.2).

2.0 Viwango vya Ukuaji kwa Shughuli za Kiuchumi

2.1 Kilimo, Misitu na Uvuvi


Shughuli hii inahusika na uvunaji wa bidhaa za mazao na wanyama. Shughuli hizi zinazojumuisha mazao ya kupandwa, ufugaji na uzalishaji wa wanyama, uvunaji wa miti na mimea mingine, wanyama au bidhaa za wanyama kutoka katika mashamba ya ufugaji au mazingira ya asili.

2.1.1 Mazao

Mazao makuu yaliyojumuishwa ni pamoja na mahindi, mpunga, ulezi/mtama, nafaka nyingine, mihogo, viazi mviringo, viazi vitamu, maharagwe, mikunde, mbegu za mafuta, mboga mboga, ndizi, matunda mengine, karanga, kahawa, pamba, chai, tumbaku na mazao mengine ya chakula na biashara.

Shughuli hii iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 2.7 katika robo ya kwanza mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 3.7 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huo ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa mazao uliotokana na matumizi ya teknolojia na pembejeo bora; kuwepo kwa hali nzuri ya hewa katika maeneo ya uzalishaji na kuimarika kwa huduma za ugani.

Kielelezo Na. 5: Uzalishaji wa Baadhi ya Mazao Robo ya Kwanza, Mwaka 2022 na 2023



Chanzo: Wizara ya Kilimo, 2023

Mazao ambayo yalichangia zaidi ukuaji wa shughuli hii katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023 ni pamoja na mkonge ambao uliongezeka kwa asilimia 16.7, mbegu za mafuta asilimia 3.0, korosho asilimia 1.4 na maharage/mikunde asilimia 0.6.

2.1.2 Mifugo

Shughuli hii inahusika na ufugaji ng'ombe wa asili na wa kisasa; mbuzi, kondoo, punda, farasi, nguruwe, sungura, kuku wa kienyeji na kisasa; na ndege wa aina nyingine.

Katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023, uzalishaji wa mifugo uliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.0 ambacho ni sawa na kiwango cha ukuaji kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huo inawezekana ulichangiwa na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za mifugo, ukuaji wa miji pamoja na kuongezeka kwa uelewa wa wananchi juu ya umuhimu wa kutumia lishe bora kutokana na mazao ya mifugo.

2.1.3 Misitu

Shughuli hii inahusisha uzalishaji na uvunaji wa mazao ya misitu kama vile magogo, mkaa, kuni, matawi ya miti, na bidhaa nyingine zisizo za miti kama vile asali na nta.

Shughuli ya misitu ilikua kwa kiwango cha asilimia 4.7 katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 3.6 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huo ulitokana na kuongezeka kwa usimamizi wa rasilimali za misitu na juhudi za Serikali katika kuhakikisha uvunaji endelevu wa bidhaa za misitu.

2.1.4 Uvuvi

Shughuli ya uvuvi inahusika na uvunaji wa rasilimali za uvuvi katika maji ya bahari na vyanzo vingine vya maji baridi.

Shughuli ya uvuvi ilikua kwa kiwango cha asilimia 0.2 katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023 ikilinganishwa na kiwango cha asilimia 5.8 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Kupungua kwa kasi ya ukuaji wa shughuli ya uvuvi ulisababishwa na mabadiliko ya tabianchi na matumizi ya vifaa duni vya uvunaji wa mazao ya uvuvi katika kipindi hicho.

2.2 Uchimbaji Madini na Mawe

Shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe inahusisha uchimbaji au ukusanyaji wa madini katika hali zake za yabisi kama vile makaa ya mawe, vimiminika (mfano petroli) au gesi (mfano gesi asilia). Uchimbaji wa madini na mawe hufanyika chini ya ardhi, ukusanyaji juu ya ardhi au kwenye visima. Uchimbaji wa madini na mawe pia unajumuisha shughuli za ziada zinazolenga kutayarisha madini kwa ajili ya kuuzwa, kwa mfano, kusaga, kusafisha na kukausha. Shughuli hizi mara nyingi zinafanywa na vitengo ambavyo vinavuna rasilimali za madini / au nyingine zilizopo karibu na migodi.

Shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe imegawanyika katika maeneo makuu manne ambayo ni:

- 1) Madini ya makaa ya mawe;
- 2) Petroli na gesi asilia;
- 3) Uchimbaji wa madini ya chuma; na
- 4) Madini ya kokoto na mawe.

Katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023, shughuli ya uchimbaji wa madini na mawe iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 14.2 ikilinganishwa na asilimia 9.7 kipindi kama hicho mwaka 2022. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa madini baadhi ya madini yaliyoongezeka zaidi yalikuwa makaa ya mawe na gesi asilia. Katika robo ya kwanza mwaka 2023, uzalishaji wa makaa ya mawe uliongezeka hadi tani 875,818 ikilinganishwa na tani 452,071 kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, kiasi cha gesi asilia kilichozalishwa kiliongezeka hadi mita za ujazo milioni 20,858 katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023 kutoka mita za ujazo milioni 18,401 kipindi kama hicho mwaka 2022 (*Jedwali Na. 1*)

Jedwali Na. 1: Uzalishaji wa Madini Robo ya Kwanza, Mwaka 2019 – 2023

Madini	Kipimo	2019	2020	2021	2022	2023
Jasi	Tani	75,593	72,390	140,376	120,168	145,817
Makaa ya Mawe	Tani	205,045	160,855	190,932	452,071	875,818
Pozollana	Tani	74,514	31,353	34,608	70,411	82,553
Gesi asilia	Mscf	16,138	14,573	14,432	18,401	20,858

Chanzo: Wizara ya Madini 2023

2.3 Uzalishaji Viwandani

Shughuli ya uzalishaji viwandani inahusisha uchakataji wa bidhaa kutoka katika hali yake ya kawaida na kuzalisha bidhaa za aina nyingine ambazo zinaweza kutumika moja kwa moja na mlaji wa mwisho au kutumika kuzalisha bidhaa nyingine. Bidhaa zinazoweza kuchakatwa ni pamoja na bidhaa za kilimo, misitu, uvuvi, madini na bidhaa nyingine za viwandani.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya uzalishaji viwandani kiliongezeka hadi asilimia 6.5 katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023 kutoka asilimia 6.3 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huu ulichangiwa na ongezeko la uzalishaji wa bidhaa za viwandani.

2.4 Umeme

Shughuli hii inahusika na uzalishaji na usambazaji wa umeme na gesi asilia, kupitia miundombinu ya kudumu ya waya na mabomba. Uzalishaji wa umeme ni kutoka katika vyanzo vya maji, mafuta na gesi. Shughuli hii inahusika na usambazaji na ugawaji wa umeme. Vyanzo vikuu vya takwimu za uzalishaji wa umeme ni kutoka katika makampuni ya uzalishaji wa umeme.

Ukuaji wa shughuli ya uzalishaji wa nishati ya umeme hutegemea kiasi cha umeme kilichozalishwa na kusambazwa kwa wateja mbalimbali. Katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023, kiasi cha umeme kilichosambazwa kiliongezeka hadi saa za kilowati milioni 2,107 kutoka saa za kilowati milioni 1,949 kipindi kama hicho mwaka 2022.

Aidha, shughuli ya uzalishaji umeme ilikua kwa kiwango cha asilimia 8.1 katika robo ya kwanza mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 8.3 kipindi kama hicho mwaka 2022.


2.5 Usambazaji Maji

Shughuli hii inahusika na kukusanya na kusafisha maji kwa ajili ya ugavi, kusafisha maji ya bahari kwa kuondoa chumvi ili kuzalisha maji ya kutumia kama bidhaa kuu na kukusanya maji moja kwa moja kutoka katika visima kwa ajili ya matumizi ya makampuni ya maji au matumizi binafsi katika kilimo au kaya. Vilevile, shughuli hii inahusika na ukusanyaji wa maji taka.

Kiashiria cha kuongezeka kwa kiwango cha ukuaji wa shughuli ya usambazaji maji ni kiasi cha maji kilichozalishwa. Katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023, kiasi cha maji kilichozalishwa kiliongezeka hadi mita za ujazo milioni 91.7 kutoka mita za ujazo milioni 86.9 zilizozalishwa kipindi kama hicho mwaka 2022.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya usambazaji maji kilikuwa asilimia 5.1 katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 11.9 kipindi kama hicho mwaka 2022.

Kielelezo Na. 6: Uzalishaji Maji (Mita za Ujazi Milioni) Robo ya Kwanza, Mwaka 2019 – 2023



Chanzo: Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji

2.6 Ujenzi

Shughuli hii inajumuisha ujenzi wa aina zote na shughuli maalum za ujenzi kwa ajili ya majengo na kazi za uhandisi. Shughuli hii inajumuisha pia ujenzi mpya, ukarabati, kufanya mabadiliko makubwa kwenye majengo na ujenzi wa miundombinu.

Shughuli za ujenzi zinajumuisha, ujenzi wa nyumba za makazi, ujenzi wa majengo ya biashara au ofisi, maduka na majengo mengine ya umma na miundombinu ya mashambani. Shughuli hii pia unajumuisha ujenzi wa barabara, madaraja, reli, viwanja vya ndege, bandari na miundombinu ya maji, mifumo ya umwagiliaji, mifumo ya majitaka, miundombinu ya viwanda, mabomba, mifumo ya umeme na vituo vya michezo.

Katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023, shughuli ya ujenzi iliongezeka hadi kiwango cha asilimia 6.2 kutoka asilimia 5.4 kipindi kama hicho mwaka 2022. Tathmini ya ukuaji wa shughuli ya ujenzi hutumia viashiria vya uzalishaji wa bidhaa za ndani ya nchi zinazotumika katika ujenzi. Bidhaa za ndani zilizochangia ukuaji wa shughuli hii ni pamoja na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za chuma.

2.7 Biashara na Matengenezo

Shughuli hii inajumuisha uuzaji wa jumla na rejareja (uuzaji wa bidhaa bila ya kufanya mabadiliko) wa aina yoyote ya bidhaa, pamoja na utoaji wa huduma kwa ajili ya uuzaji wa bidhaa. Pia inahusisha ukarabati wa magari na usimikaji wa mitambo na ukarabati wa bidhaa binafsi za nyumbani. Shughuli kuu ni kununua na kuuza bidhaa.

Ukuaji wa shughuli ya biashara na matengenezo iliongezeka hadi asilimia 6.0 katika robo ya kwanza mwaka 2023 kutoka asilimia 5.9 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji wa shughuli hii ulichangiwa na kuongezeka kwa bidhaa zilizouzwa ikiwa ni pamoja na bidhaa za kilimo, bidhaa zilizozalishwa viwandani na zilizoagizwa kutoka nje ya nchi.

2.8 Uchukuzi na Uhifadhi wa Mizigo

Shughuli hii inahusisha utoaji wa huduma ya usafiri wa abiria au/na mizigo, ikiwa ni kwa ratiba maalum au isiyokuwa na ratiba, kwa njia ya reli, bomba, barabara, maji au anga na shughuli zinazohusiana ikiwa ni pamoja na utunzaji wa mizigo na uhifadhi. Shughuli hii pia inajumuisha kukodisha vifaa vya usafiri na madereva na shughuli za posta na usafirishaji wa vifurushi.

Kasi ya ukuaji wa shughuli ya uchukuzi na uhifadhi wa mizigo iliongezeka hadi kiwango cha asilimia 2.3 katika robo ya kwanza mwaka 2023 kutoka asilimia 1.3 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huu umetokana na kuongezeka kwa idadi ya abiria na mizigo iliyosafirishwa kwa njia ya barabara katika kipindi hicho.

2.9 Malazi na Huduma za Chakula

Shughuli hii inajumuisha utoaji huduma ya makazi ya muda mfupi kwa wageni na wasafiri wengine na utoaji wa huduma ya chakula na vinywaji kwa mlaji wa mwisho.

Shughuli ya malazi na huduma za chakula iliongezeka hadi kiwango cha asilimia 12.3 katika robo ya kwanza mwaka 2023 kutoka asilimia 1.5 kipindi kama hicho mwaka 2022. Kasi ya ukuaji wa shughuli ya malazi na huduma za chakula katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023 ilichangiwa na kuongezeka kwa idadi ya watalii walioingia nchini ambao walifikia 409,082 kutoka watalii 289,372 walioingia nchini kipindi kama hicho mwaka 2022.

2.10 Habari na Mawasiliano

Shughuli hii inahusika na uchapishaji, upigaji picha za kawaida, picha za video na uzalishaji wa programu za televisheni, kurekodi sauti na kuchapisha muziki, shughuli za programu na utangazaji kwa mfano utangazaji wa redio na televisheni, mawasiliano ya simu, programu za kompyuta, ushauri na shughuli zinazohusiana na shughuli za huduma za habari kama vile uchakataji wa taarifa.


Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya habari na mawasiliano kiliongezeka hadi asilimia 6.4 katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023 kutoka asilimia 6.3 kipindi kama hicho mwaka 2022. Kasi ya ukuaji ilichangiwa na kuongezeka kwa muda wa maongezi, huduma za ujumbe mfupi uliotumwa na kuongezeka kwa idadi ya wateja waliopata huduma za fedha kupitia mitandao ya simu pamoja na huduma za utangazaji na huduma za inteneti kwa ujumla.

2.11 Fedha na Bima

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za fedha, bima, pensheni ya hiari, na huduma nyingine za fedha.

Huduma ya fedha na bima iliongezeka hadi kiwango cha asilimia 12.9 katika robo ya kwanza mwaka 2023 kutoka asilimia 8.8 katika robo ya kwanza mwaka 2022. Ukuaji wa shughuli ya fedha na bima ilichangiwa na kuongezeka kwa asilimia 19.2 kwa amana za wateja kutoka shilingi trilioni 26.6 mwaka 2022 hadi shilingi trilioni 31.7 mwaka 2023; kuongezeka kwa asilimia 23.1 kwa mikopo kutoka shilingi trilioni 22.9 mwaka 2022 hadi shilingi trilioni 28.2 mwaka 2023.

Kielelezo Na. 7: Thamani ya Mikopo na Amana (Sh. Trilioni), Robo ya Kwanza, Mwaka 2019 – 2023



Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania

2.12 Upangishaji Majengo

Shughuli hii inahusika na utoaji wa huduma za kuuza au kununua majengo, kukodisha mali, majengo na pia kutoa huduma nyingine za mali isiyohamishika ikiwa ni pamoja na kupima mali isiyohamishika kama vile viwanja.

Kiwango cha ukuaji wa shughuli ya upangishaji majengo kiliongezeka kwa asilimia 4.1 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 4.5 kipindi kama hicho mwaka 2022. Ongezeko la mahitaji ya huduma za malazi hususan katika maeneo ya mjini lilichangia ukuaji wa shughuli hii ya uchumi.

2.13 Shughuli za Kitaalam, Ufundi na Sayansi

Shughuli hii inajumuisha shughuli maalum za kitalaam, kisayansi na kiufundi. Shughuli hizi zinahitaji kiwango cha juu cha mafunzo, pamoja na kupata ujuzi maalum unaotumika kutoa huduma kwa watumiaji. Shughuli hii inahusisha huduma za kisheria na uhasibu; ushauri na usimamizi; usanifu na uhandisi; kupima na uchambuzi wa kitaalam; utafiti wa kisayansi na maendeleo; matangazo na utafiti wa masoko; utaalam wa aina nyingine wa kisayansi na kiufundi pamoja na shughuli za ugani.

Kasi ya ukuaji wa shughuli za kitaalam, kisanyansi na kiufundi iliongezeka hadi asilimia 5.3 katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023 kutoka asilimia 5.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Huduma za kisheria na uhasibu zilichangia katika kiwango cha ukuaji uliofikiwa.

2.14 Huduma Zinazohusiana na Utawala

Shughuli hii inajumuisha huduma mbalimbali zinazosaidia kufanyika kwa biashara ambazo ni huduma za: kukodisha vifaa, ajira, uwakala wa kampuni za usafiri, kuongoza watalii, kuandaa malazi; na huduma nyingine zinazohusiana na usalama na uchunguzi; pamoja na huduma kwenye majengo na uboreshaji wa mazingira.

Kiwango cha ukuaji wa Huduma zinazohusiana na Utawala kiliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.5 katika robo ya kwanza mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 6.0 kipindi kama hicho mwaka 2022. Kuongezeka kwa huduma za uwakala wa usafiri wa watalii ulichangia zaidi ukuaji wa shughuli hii ya kiuchumi.

2.15 Utawala na Ulinzi

Shughuli ya Utawala na Ulinzi inahusika na kutunga na kutafsiri sheria, kukusanya kodi, ulinzi wa mipaka ya nchi, usalama wa raia na mali zao, huduma za uhamiaji, pamoja na uendeshaji wa Serikali kwa ujumla. Aidha, huduma za mifuko ya hifadhi ya jamii ya lazima imejumuishwa katika shughuli ya Utawala na Ulinzi.

Kasi ya ukuaji wa shughuli ya utawala na ulinzi iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 3.7 katika robo ya kwanza mwaka 2023 ikilinganishwa na asilima 5.6 kipindi kama hicho mwaka 2022. Kiwango cha ukuaji kilitokana na kuongezeka kwa matumizi ya fedha za Serikali katika mishahara, kulipa malimbikizo ya madai ya wafanyakazi na utekelezaji wa kazi za ulinzi na usalama pamoja na uendeshaji wa Serikali kwa ujumla.

2.16 Elimu

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa elimu katika ngazi zote, kwa njia ya kuongea au maandishi au kwa njia ya redio na televisheni au njia nyingine za mawasiliano. Vilevile, inajumuisha elimu inayotolewa na taasisi mbalimbali katika mfumo wa kawaida wa shule katika ngazi tofauti pamoja na elimu ya watu wazima na elimu ya kujifunza kusoma na kuandika. Shughuli hii inajumuisha elimu katika sekta ya umma na binafsi.

Shughuli ya elimu iliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.9 katika robo ya kwanza mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 6.5 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji wa shughuli hii umetokana na udahili wa wanafunzi katika ngazi zote za utoaji wa elimu za umma na binafsi ikiwa ni pamoja na kuongezeka kwa mishahara na matumizi ya Serikali katika utoaji wa elimu bila ada.

2.17 Afya

Shughuli hii inajumuisha utoaji wa huduma za afya na maendeleo ya jamii. Inajumuisha pia huduma za afya zinazotolewa na wataalam wa matibabu katika hospitali na vituo vingine, shughuli nyingine za huduma za makazi ambazo zinahusisha shughuli za huduma za afya kwa jamii bila ushirikishwaji wa wataalam wa huduma za afya.

Shughuli ya utoaji wa huduma za afya iliongezeka kwa kasi ya asilimia 4.5 katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 5.0 katika kipindi kama hicho mwaka 2022. Ukuaji huu ulitokana na kuendelea kuboreshwa kwa huduma za utoaji wa huduma za afya kwa jamii katika ngazi zote za kutolea huduma katika vituo vya umma na binafsi na kuongezeka kwa ya mishahara ya watumishi wa umma.

2.18 Huduma Nyingine za Jamii

Shughuli hii inajumuisha shughuli za mashirika ya uanachama, ukarabati wa vifaa vya kieletroniki na bidhaa za kibinafsi za nyumbani na shughuli mbalimbali za huduma za binafsi ambazo hazijumuishwi kwenye shughuli nyingine. Pia inajumuisha shughuli ya sanaa na burudani na shughuli za kaya katika kuajiri.

Kasi ya ukuaji wa shughuli ya huduma nyingine za jamii iliongezeka hadi kiwango cha asilimia 9.5 katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023 kutoka asilimia 8.5 kipindi kama hicho mwaka 2022. Kuongezeka kwa watalii, idadi ya watu katika maeneo ya mjini na mahitaji ya huduma za jamii kulichangia ukuaji wa shughuli hii ya kiuchumi.

3.0 Hitimisho

Katika kipindi cha robo ya kwanza mwaka 2023, Pato halisi la Taifa liliongezeka kwa kiwango cha asilimia 5.6 ikilinganishwa na asilimia 5.5 kipindi kama hicho mwaka 2022. Aidha, shughuli zilizokuwa na mchango mkubwa katika ukuaji wa asilimia 5.6 ni pamoja na: uchimbaji wa madini na mawe iliyoongoza kwa ukuaji wa asilimia 14.2, ikifuatiwa na fedha na bima (asilimia 12.9), na huduma ya chakula na malazi (asilimia 12.3). Vilevile, shughuli zilizoongezeka kwa kiwango kikubwa zilikuwa: uchimbaji wa madini na mawe (asilimia 14.2); fedha na bima (asilimia 12.9); malazi na huduma za chakula (asilimia 12.3); huduma nyingine za jamii (asilimia 9.5); na usambazaji umeme (asilimia 8.1).

Kiambatisho Na. 1: Pato la Taifa kwa Shughuli za Kiuchumi kwa Bei za Mwaka 2015 – Sh. Milioni

Mwaka	Nusu Mwaka	kilimo	Madini na Mawe	Viwanda	Umeme	Maji safi na maji taka	Ujenzi	Biashara na Matengenezo	Malazi na Huduma ya Chakula	Uchukuzi na Uhifadhi Mizigo	Habari na Mawasiliano	Fedha na Bima
2014		23,952,077	3,687,273	6,919,794	815,297	381,760	9,253,082	8,444,243	1,397,782	6,577,706	1,560,064	3,764,113
2015		25,234,560	4,055,619	7,411,672	798,801	390,758	10,446,797	8,747,862	1,421,916	6,929,895	1,681,098	4,189,021
2016		26,436,338	4,356,709	8,213,364	869,262	417,899	11,960,720	9,260,703	1,480,052	7,324,856	1,718,548	4,235,515
2017		27,999,287	4,588,624	8,889,818	877,667	444,660	13,765,005	9,820,627	1,525,619	7,815,845	1,824,472	4,115,393
2018		29,504,246	4,659,195	9,623,501	928,174	477,510	15,655,747	10,396,754	1,604,391	8,736,561	1,989,716	4,094,972
2019		30,802,708	5,485,112	10,184,558	994,879	510,411	17,802,021	10,965,088	1,645,950	9,493,191	2,133,313	4,281,167
2020		32,323,885	5,887,452	10,646,279	1,049,610	540,159	19,421,672	11,196,820	1,419,654	10,293,276	2,313,029	4,412,967
2021		33,587,556	6,442,881	11,155,762	1,154,204	575,213	20,249,939	11,590,506	1,514,711	10,658,344	2,524,564	4,629,490
2022		34,711,277	7,146,141	11,624,144	1,242,132	606,754	21,131,032	12,046,448	1,651,099	11,061,950	2,712,411	5,024,141
2012	1	5,972,854	845,470	1,528,195	151,473	86,422	1,816,993	1,877,418	321,003	1,208,445	281,981	849,590
	2	5,182,996	825,383	1,544,666	164,427	89,319	1,808,760	1,855,404	320,427	1,456,176	303,507	844,631
	3	4,092,001	833,592	1,499,895	172,946	92,526	2,012,312	1,725,714	358,248	1,489,645	327,526	886,247
	4	6,559,178	810,297	1,494,233	180,223	90,094	1,940,197	1,912,875	344,245	1,556,199	353,733	863,692
2013	1	5,994,220	748,412	1,459,422	167,460	87,306	2,146,785	1,828,162	332,454	1,519,508	312,238	811,387
	2	5,376,452	850,463	1,547,040	177,004	90,069	2,111,891	1,884,307	324,659	1,501,581	343,060	836,571
	3	4,199,755	875,290	1,677,731	181,477	85,918	2,389,873	1,893,295	354,104	1,513,039	358,452	881,698
	4	6,837,765	990,556	1,608,322	197,667	104,598	2,374,804	2,076,522	344,987	1,516,849	400,366	876,284
2014	1	6,335,448	937,448	1,621,405	201,849	87,893	2,182,230	2,054,479	346,623	1,625,429	342,909	912,095
	2	5,877,120	871,899	1,706,772	182,845	94,708	2,507,336	2,073,942	339,327	1,616,710	380,305	927,895
	3	4,450,294	929,381	1,788,128	213,998	97,099	2,228,708	2,035,245	361,470	1,686,150	414,058	960,721
	4	7,289,215	948,546	1,803,489	216,605	102,059	2,334,808	2,280,578	350,362	1,649,417	422,793	963,401
2015	1	6,605,887	923,326	1,733,636	211,828	96,862	2,438,046	2,093,973	346,778	1,654,599	386,446	995,846
	2	6,347,239	965,335	1,820,111	199,281	92,862	2,690,105	2,195,254	345,054	1,676,064	412,841	1,011,653
	3	4,656,388	960,427	1,939,664	192,215	99,585	2,601,253	2,162,776	372,080	1,764,202	441,478	1,076,143
	4	7,625,045	1,206,532	1,918,260	195,477	101,448	2,717,393	2,295,860	358,003	1,835,030	440,334	1,105,380
2016	1	6,788,342	1,017,609	1,965,656	214,850	95,779	2,859,933	2,295,506	358,142	1,818,390	401,047	1,111,056
	2	6,853,095	1,109,064	1,996,019	210,034	100,816	2,995,869	2,318,553	347,167	1,819,827	421,552	1,052,954
	3	4,936,684	1,098,979	2,080,908	214,673	103,584	3,208,669	2,300,383	385,323	1,854,653	451,160	1,053,955
	4	7,858,218	1,131,055	2,170,783	229,706	117,720	2,896,249	2,346,262	389,420	1,831,986	444,789	1,017,550
2017	1	7,232,707	1,118,373	2,067,899	223,828	97,295	3,204,078	2,338,463	374,854	1,914,669	451,530	1,046,358
	2	7,283,410	1,057,691	2,187,504	207,472	105,045	3,631,267	2,437,207	359,355	1,910,951	448,738	1,028,325
	3	5,137,218	1,144,597	2,365,766	222,983	113,969	3,198,026	2,434,184	395,146	1,982,315	459,599	998,075
	4	8,345,952	1,267,964	2,268,650	223,383	128,352	3,731,635	2,610,773	396,263	2,007,909	464,604	1,042,635
2018	1	7,717,810	1,054,655	2,173,169	225,308	100,913	3,703,467	2,436,626	391,664	2,082,426	522,213	1,017,349
	2	7,716,375	1,129,287	2,259,893	221,254	111,470	3,846,566	2,528,958	383,333	2,169,733	506,999	1,004,546
	3	5,333,861	1,166,716	2,530,756	235,525	126,137	3,711,275	2,601,456	425,407	2,222,813	481,218	1,036,219
	4	8,736,201	1,308,537	2,659,683	246,088	138,991	4,394,440	2,829,714	403,987	2,261,589	479,286	1,036,859
2019	1	8,139,275	1,159,804	2,280,570	249,013	108,984	4,201,084	2,529,025	390,255	2,312,794	563,309	1,069,349
	2	8,039,478	1,323,857	2,384,031	239,855	118,551	4,636,133	2,673,618	393,345	2,322,004	538,298	1,046,826
	3	5,485,725	1,413,025	2,749,036	247,875	139,826	4,350,024	2,794,017	442,538	2,407,844	516,819	1,084,998
	4	9,138,231	1,588,425	2,770,921	258,136	143,049	4,614,781	2,968,428	419,812	2,450,548	514,887	1,079,995
2020	1	8,469,003	1,365,988	2,387,165	264,424	116,821	4,408,146	2,650,981	400,323	2,505,607	610,395	1,114,722
	2	8,366,922	1,438,625	2,479,030	247,858	124,044	5,203,762	2,668,493	330,902	2,541,456	592,499	1,078,981
	3	5,838,125	1,491,966	2,882,547	258,781	150,811	4,955,258	2,852,399	331,271	2,576,818	560,949	1,105,924
	4	9,649,835	1,590,872	2,897,536	278,547	148,483	4,854,506	3,024,946	357,157	2,669,394	549,186	1,113,341
2021	1	8,694,642	1,489,458	2,532,535	283,588	127,311	4,641,094	2,768,552	374,418	2,730,301	661,347	1,144,304
	2	8,585,645	1,574,503	2,589,415	277,917	134,491	5,302,015	2,783,463	364,386	2,666,798	659,757	1,119,611
	3	6,140,943	1,677,259	2,995,394	284,691	157,663	5,241,139	2,905,381	378,526	2,560,195	607,521	1,158,549
